## BETHLEHEM WORSHIP CENTRE



*Mtumishi wa Mungu Mchungaji Arthur Mulungu na Mkewe Exaveria Mlowe ndio Waanzilishi wa Huduma ya BWC wakiwa na Kauli mbiu ya kuwekeza Huduma yenye Vipaumbele katika mafundisho sahihi na Neno la Mungu, Maombi pamoja, Kumtumikia Mungu na Kumwabudu Mungu katika viwango vya juu. Fuatana Na Mtumishi wa Mungu*

**Mchungaji Arthur na Exaveria Mulungu wanapenda kukukaribisha kwenye Ibada za upako wa Roho mtakatifu ili uweze kushiriki Nasi Baraka za Mungu.**

## UNDERSTANDING BETHLEHEM WORSHIP CENTRE

*Kufahamu kituo cha kumwabudu Mungu cha Bethlehem*

**UTANGULIZI**

1. **BETHLEHEM**

**BETHLEHEM:**

*Huitwa Mji wa Daudi (The city of David), kwa sababu alizaliwa hapa sambamba na Mji aliozaliwa Yesu Kristo toka kabila la Yuda, Ni mji uliokuwa maili sita magharibi mwa Jerusalem.*

**1.1 BETH-EL + LEHEM**

Kwa tafsiri ya Kiebrania, katika Tamaduni za Kiyahudi na Lugha ya Armain ndiyo pia ilitumika katika kuandika magombo ya Agano la Kale kwa sehemu kubwa. Neno hili linaundwa na maneno Matatu Makubwa.

1. Beth: Mahali / Nyumba
2. Eli: Mungu
3. Lehem: Mkate / Mikate




1 + 2 = **Betheli** = Nyumba ya Mungu | Mahali alipo ama anapatikana Mungu

**Betheli**, jina la mji wa magharibi wa Ai, kwenye mipaka ya makabila ya Efraimu na Benyamini, Mwa 12:8; 28:10-22, na kuchukua mahali ambapo Yakobo alilala na kuota ndoto yake ya kukumbukwa, jina aliloipa kisha likapita jina la zamani **Luzu,** Amu 1:23

Huitwa nyumba ya Mungu yenye mkate | Mahali unapopatikana mkate | Mahali anapopatikana Mungu ili kutuhudumia chakula cha uzima. *Mathayo 4:4 Naye akajibu akasema, Imeandikwa, Mtu hataishi kwa* ***mkate*** *tu, ila kwa kila* ***neno*** *litokalo katika kinywa cha Mungu.*

*Waebrania 4:12 Maana* ***Neno la Mungu*** *li hai, tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake; tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo.*

*1 Wak 11:223-27 Kwa maana mimi nalipokea kwa Bwana niliyowapa nanyi, ya kuwa Bwana Yesu usiku ule aliotolewa alitwaa mkate, naye akiisha kushukuru akaumega, akasema, Huu ndio mwili wangu ulio kwa ajili yenu; fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu. Na vivi hivi baada ya kula akakitwaa kikombe, akisema, Kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu; fanyeni hivi kila mnywapo, kwa ukumbusho wangu. Maana kila mwulapo mkate huu na kukinywea kikombe hiki, mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo. Basi kila aulaye mkate huo, au kukinywea kikombe hicho cha Bwana isivyostahili, atakuwa amejipatia hatia ya mwili na damu ya Bwana.*

*Mika 5: 2 Bali wewe,* ***Bethlehemu*** *Efrata, uliye mdogo kuwa miongoni mwa elfu za Yuda; kutoka kwako wewe atanitokea mmoja atakayekuwa mtawala katika Israeli; ambaye matokeo yake yamekuwa tangu zamani za kale, tangu milele.*

Mji ambapo alipozaliwa Daudi na Kristo Mwokozi wetu toka katika kabila la Yuda, maili sita kusini magharibi mwa Yerusalemu.

***Mifano michache ya kila unapoona neno Beth ujue Ni mahali Na EL ama ELI Ujue Ni Jehova***

a. **BETHE-SDA = Nyumba ya Rehema =** ***House of MERCY***

Jina la bwawa ama birika au chemchemi karibu na hekalu la Yerusalemu, mahali ambapo wagonjwa walikuja kujaribu kuponywa magonjwa yao.Yoh 5:2.

b. **BETH-PHAGE** - Place of figs, Mahali pa tini, kijiji kidogo upande wa mashariki wa Mlima wa Mizeituni, karibu na Bethania, Mt 21:1; Mk 11:1; Lu 19:29.

c. **BETH-SAIDA**

Place of fishing, Mahali pa kuvua samaki, Mji katika Galilaya, kwenye ufuo wa magharibi wa ziwa la Genesareti, kaskazini kidogo ya Kapernaumu; palikuwa mahali pa kuzaliwa kwa mitume Filipo, Andrea, na Petro, na mara nyingi alitembelewa na Bwana wetu, Mt 11:21; Mk 6:45; 8:22.

d. **BETH-SHEMESH**

House of the sun, Mji wa Yuda walikokuwa Makuhani,

e. **ELI**

**Jina la Mungu (Jehova)**

Kuhani mkuu wa Wayahudi wakati sanduku la agano la Mungu lilikuwa Shilo, wa kwanza wa ukoo wa Ithamari, 1Sam 2:27. Pia alikuwa mwamuzi wa Israeli kwa miaka arobaini, na alikuwa maarufu kwa uchaji Mungu na Maarifa, lakini kwa kosa la jinai alipuuza nidhamu ya familia. Kwa ajili hiyo hukumu za Mungu ziliiangukia nyumba yake, 1Sam 3:11-18. Katika vita na Wafilisti wanawe wawili waliuawa, na Israeli wakashindwa; bali kukamatwa kwa sanduku la Mungu ndiko kulikovunja moyo wake, 1Sam 4:1-22, Tishio la kimungu lilifanyika kikamilifu katika siku ya Abiathari, ambayo unaona.

Wanawe, Hofni na Finehasi walijiendesha vibaya sana, na kuwachukiza sana watu (1Sam 2:27-36). Walikuwa makafiri wachafu. Alishindwa kuwakemea vikali kama vile alivyopaswa kufanya, na hivyo kuleta juu ya nyumba yake hukumu ya Mungu (1Sam 2:22-33; 3:18).

**f.** Emmanu-**eli** = Mungu Pamoja nasi

*Mithali 22:6 Mlee mtoto katika njia impasayo, Naye hataiacha, hata atakapokuwa mzee.*

Katika kila unapoona Jina la mtu katika Biblia Linaanza na ELI ujue huyo mtu alitembea na Mungu ama alitoka familia ya Kikuhani kwa maana ya kuhani Mkuu ama ni mtumishi wa Jehova. Mfano: Eli, Eliabu, c. Eliam (Gods people), Eliada (God Cares), Eliakim (God raises up), Eliashib (God Restores), Elizabeth (Mungu wa agano), Eliphaz (God is strength), Elihu (is God), Eliya (God is Jehova), Elisha (God of salvation), Elishama (God Hears), Elikana (God created)

**1.2 LEHEM = Mkate = THE BREAD**

Neno ambalo katika Maandiko mara nyingi huwekwa kama chakula cha roho.

**Mana** inaitwa mkate kutoka mbinguni, **Kut 16:4;** Mkate, kwa maana ifaayo na halisi, kwa kawaida humaanisha keki zilizotengenezwa kwa unga wa ngano; kwa shida sana kutumiwa na maskini na kulisha farasi. Ngano ilisagwa kila siku, katika mawe madogo ya kusagia; unga ulifanywa kuwa unga katika bakuli la mbao, na hatimaye kutiwa chachu, Kut 12:34; Mwanzo 7:4, Kisha ikatengenezwa keki, na kuoka.

Nb: Huu si mwanzo wa Keki ya UPAKO

***MKATE***

*Yohana 14:23 Yesu akajibu, akamwambia, Mtu akinipenda, atalishika neno langu; na Baba yangu atampenda; nasi tutakuja kwake, na kufanya makao kwake.*

- Neno la Mungu kwa maana ya Maandiko matakatifu.
- Mafundisho ya neno la Mungu.
- Maandiko mengine ya watumishi waliotumiwa na Mungu wakaandika mafunuo yao na kutunza kwenye vitabu.
- Neno la Mungu litokalo kwa mtu wa Mungu unapozungumza nae ukapata ufunuo na maarifa ya kutatua jambo lako.

***MAFUNDISHO***

- Kumjua Mungu na Ufalme wake

- Kujua makusudi yake juu yetu na kanisa lake
- Kujua namna ya Kuishi na Imani yetu katika dunia yenye uharibifu

*Mithali 8:10-11 Pokea **mafundisho** yangu, wala si fedha, Na **maarifa** kuliko dhahabu safi. Maana **hekima** ni bora kuliko marijani; Wala vyote vinavyotamanika havilingani nayo.*

**1.3 THAMANI YA NENO NA MAFUNDISHO**

## Kujifunza mambo yafuatayo:-

- **Kumtegemea na Kumwamini Mungu:** Ndiyo Msingi wa kila kitu lakini Kumtegemea Mwanadamu una expiring date. Kumtegemea Mungu hakuna mipaka lakini mwanadamu ni pale tu angalipo mtoto pekee yaani akiwa chini ya wazazi <18 years kisheria.

- *Yer 17:5-7 Bwana asema hivi, Amelaaniwa mtu yule amtegemeaye mwanadamu, Amfanyaye mwanadamu kuwa kinga yake Na moyoni mwake amemwacha Bwana. Maana atakuwa kama fukara nyikani, Hataona yatakapotokea mema; Bali atakaa jangwani palipo ukame, Katika nchi ya chumvi isiyokaliwa na watu. Amebarikiwa mtu yule anayemtegemea Bwana, Ambaye Bwana ni tumaini lake*.

  *Waebrania 5:12 Kwa maana, iwapasapo kuwa waalimu, (maana wakati mwingi umepita), mnahitaji kufundishwa na mtu mafundisho ya kwanza ya maneno ya Mungu; nanyi mmekuwa mnahitaji maziwa wala si chakula kigumu.*

- **Kujitegemea:** Ukija mjua Mungu na unaweza kumtegemea kuna baadhi ya mambo Mungu atataka ukue kiroho na hivyo utoke kwenye daraja la kuamini katika kuombewa na kuanza kujiombea mwenyewe. Toka kusomewa maandiko matakatifu ama kuazima Bibilia na kununua na kumiliki Biblia yako takatifu. Lakini katika mambo yote Kumtegemea Mungu ndiyo Msingi wa kanuni zote.

  *Waebrania 5:14 Lakini chakula kigumu ni cha watu wazima, ambao akili zao, kwa kutumiwa, zimezoezwa kupambanua mema na mabaya.*

  *1 Wakorintho 14:20 Ndugu zangu, msiwe watoto katika akili zenu; lakini katika uovu mgeuzwe watoto wachanga, bali katika akili zenu mkawe watu wazima.*

  *Mathayo 24:4 Yesu akajibu, akawaambia, Angalieni, mtu asiwadanganye.*

- **Kutegemewa:** Huwezi kutegemewa ikiwa unategemea. Kwa hiyo Mtu anayemtegemea Mungu, akikua na kuanza kujitegemea baadae atakuwa mtu mzima yaani anategemewa na Jamii yake, Mungu na Taifa pia.

  *Luka 22:32 lakini nimekuombea wewe ili imani yako isitindike; nawe utakapoongoka waimarishe ndugu zako.*

  *Warumi 8:28 Nasi twajua ya kuwa katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema, yaani, wale walioitwa kwa kusudi lake.*


*Marko 16:15 Akawaambia, Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe*

*BWC inawaanda watu kumtegemea Mungu, Kuweza kujitegemea na kuwaanda kuja kuwa watu wa kutegemewa na kuwa na uwezo wa kutunza familia zao na jamii nyingine.*

## 2. IBADA (FELLOWSHIP)

**Utangulizi:** Ni tendo la heshima ya hali ya juu linalofanywa na mtu kwa kiumbe aliye mkuu katika mazingira yake yote, kiroho na kimwili na kiumbe huyo akaaminiwa kuwa ni MWENYE ENZI asiyefananishwa na kiumbe kingine mkamilifu katika matendo yake. Kuabudu Mungu katika Roho na Kweli kunaweza kukafanywa wakati wowote na mahali popote mradi lengo ni kumfanyia Mungu IBADA.Jambo la muhimu ni yule tunayemwabudu kuliko mahali tunapofanyia ibada ingawa mahali tunafanyia ibada ni kitu chema,lakini pasipewe nafasi mioyoni mwetu na kuheshimiwa kama sehemu ya ibada.Pamoja na hoja hiyo mahali pa ibada pasipuzwe na kudharauliwa maana pamewekwa wakfu kwa huduma ya Mungu pametakaswa . Mtu akionyesha dharau au kuto paheshimu anaweza kupata madhara, hivyo ni muhimu kila mtu ajue jambo hili na kuenenda kwa utaratibu na kwa heshima mahali hapo.Kwa vile Ibada ni shughuli ambayo inashikamana sana na mfumo wa maisha ya mwanadamu, na kwamba ibada hutofautiana sana katika maana na mitazamo kulingana na imani ya mtu juu ya Mungu anayemwabudu, ni vema tukaelewa kwa usahihi ibada ninini kwa mujibu wa Biblia ifundishavyo.
Rum 12:1-2 Tendo la Ibada ni tendo la kujitoa kama dhabihu, lakini ibada ya kweli lazima dhabihu hiyo iwe hai na takatifu, Mwili, Roho na ufahamu viwe na lengo moja lakumfanyia Mungu Ibada takatifu basi, ambapo ibada nje ya utakatifu si ibada inayompendeza.









## 2.1 MAANA YA IBADA

Ibada ni kumshangaa Mungu. Kwa ufahamu tulio nao na akili ya kibinadamu tuliyo nayo hatuwezi kumwelewa Mungu kikamilifu tukamfahamu. *Isaya 55:8-9: "Maana mawazo yangu si mawazo yenu, wala njia zenu si njia zangu; asema BWANA*. Kwa maana kama vile mbingu zilivyo juu sana kuliko nchi, kadhalika njia zangu zi juu sana kuliko njia zenu, na mawazo yangu kuliko mawazo yenu." Mungu ni mkuu kuliko uwezo wa ufahamu wa mwanadamu na yuko juu sana kuliko mawazo ya mwanadamu na yuko juu sana kuliko njia za mwanadamu kwa hiyo hatuwezi kumfahamu vyema" Hivyo basi siku zote tutakapokusanyika pamoja au mtu akiwa peke yake kumwabudu na kukutana naye atamshangaa (tutamshangaa). Hutaweza kukaa mbele za Mungu ukimwabudu katika Roho na Kweli ikawa jambo la kawaida, maana Mungu huyo ni Mfalme Mkuu lazima utamshangaa Mfalme huyo. Utukufu wake utakushangaza na kutamani kumwangalia. Wafalme wa dunia japokuwa ni wanadamu, raia wao hutetemeka na kuwaheshimu wanapojitokeza mbele zao, na kila mtu hutamani kumwona na kumshangaa, na kukusanyika mahali pamoja ili wamsikilize Mfalme wao. Mungu ni Mfalme wa ajabu anayejihudhurisha kati ya watu wake wanapomfanyia ibada kwa kumwabudu na kuwashangaza waabuduo ambapo na wao wanazama katika mshangao. Zab. 47:7, 66:3, 68:35, 71:16, 89:7

## 2.2 WORSHIP / USHIRIKA NA MUNGU

*Yohana 4:24 Mungu ni Roho, nao wamwabuduo yeye imewapasa kumwabudu katika roho na kweli.*

Kusudi la Mungu kumuumba mwanadamu ni USHIRIKA (**FELLOWSHIP)** Mwanzo 1:26-27, 2:7, 21:-25, 3:8-10 Katika ushirika huo ndiko tunapata chimbuko la ibada ya mwanadamu. Mungu hawezi kufanya Ushirika na mwanadamu katika asili ya mwili moja kwa moja maana yeye ni ROHO, kwahiyo Mungu alimuumba mwanadamu kwa mfano wake, na mfano huo ni katika ROHO.

Ushirika wetu na Mungu uko katika ROHO, na kwa Roho tunafanana na Mungu. Mwanzo 2:7. Bwana Mungu akamfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi, akampulizia puani pumzi yenye uhai, mtu akawa nafsi hai. **Mwili** ni jengo au makao, hema, na kifuniko cha Roho ambayo ni pumzi yenye uhai, ili kwa huyo Roho Mungu ajidhihirishe kwa ulimwengu katika ufahamu wetu, Yaani mwili ambao ni mavumbi, Katika msingi huo kusudi la Mungu kutuumba linatimia. Yapo makusudi makuu mawili ambayo ni: - **Kumtumikia na Kumwabudu**. Mwanadamu awaye yote asiyefanya mambo hayo mawili amekosea lengo na kusudi la asili ya kuumbwa kwake. Katika mambo haya mawili, wajibu wa kwanza ni kuabudu, yule unayemwabudu hatimaye unamtumikia na kuyakubali matakwa yake kwa kumtumikia.

Wajibu wa kwanza wa Adamu ulikuwa ni kuabudu na siyo kuhubiri ama kufanya huduma zingine, Mungu alikuja katika ibada wakati wa jua kupunga jioni ili kufanya ushirika nao, **kuhubiri neno** ni matokeo ya anguko la Adamu kumuasi Mungu na kuacha wajibu wake wa ibada na Mungu, Msingi mkuu wa mahusiano ni Ibada. Mw 3:8 inasema wakasikia sauti ya Mungu akitembea bustanini, Hii inaonyesha kwamba Adamu alikuwa na ushirika na MUNGU kiasi cha kuzijua hatua za MUNGU alivyotembea ikiwa ni ushahidi wakutosha kwamba walikua na ushirika mzuri.

*Waebrania 10:25 wala tusiache kukusanyika pamoja, kama ilivyo desturi ya wengine; bali tuonyane; na kuzidi kufanya hivyo, kwa kadiri mwonavyo siku ile kuwa inakaribia.*

**2.3 ASILI YA KUABUDU**

Kuabudu asili yake ni mbinguni, kuabudu kulikuwepo kabla ya Adamu kuumbwa, walikuwepo viumbe kabla ya Adamu huko mbinguni waliomwabudu Mungu. Ibada asili yake ni Mungu mwenyewe, Uungu una asili ya kuabudiwa kwa hiyo chanzo cha ibada ni Mungu (Ayubu 38:4-7, Zaburi 148:2-14).




**KUABUDU** ni hisia za upendo mkuu kunakohusisha hisia kali zenye upendo mkuu zinazogusa ufahamu na kuzama katika upendo wa ndani kabisa na kuhusudu. (Adoration) Kuhusudu ni mguso ambao unaachilia hisia za papo kwa hapo, na kusema kwa sauti ya kusikika maneno yenye kujaa mlipuko wa upendo mkuu, na kwa sauti ya upole na kugugumiza maneno, pamoja na ubembelezi mwingi, ukiambatana na maombi yaliyojaa unyenyekevu, heshima, adabu na hofu na kujikita katika ibada ya dhati mbele ya Mungu, kumsifu na kumwabudu.

*Neh 8:5-6 Ezra akakifunua kitabu machoni pa watu wote; (maana alikuwa juu ya watu wote); na hapo alipokifungua, watu wote* ***(1) walisimama****; Ezra akamhimidi Bwana, Mungu Mkuu. Nao watu wote wakaitika, Amina, Amina, pamoja na* ***(2) kuinua mikono Yao****; kisha (3)* ***wakainama vichwa vyao****, (4)* ***wakamsujudu (****5)* ***kifudifudi Bwana.***

**2.4 MAANA KAMILI YA KUABUDU**

Maana yake ni tendo linalogusa akili, hisia, nafsi na utu wa mtu na mwili pia kwa kusujudu, kuanguka kifudifudi au uso kwa uso. Mw. 17:3 Tendo hili linafanywa pasipo ushawishi wa kitu, wala si nje ya Moyo wa kumtambua Mungu kuwa wa thamani kuliko kitu chochote anayestahili kupewa ibada ya pekee na kupelekea kujitoa kwake bila unafiki wala ubinafsi. Ni dhana zaidi ya ufahamu wetu, taratibu, desturi na mipango ya ibada. Ni ibada inayojumuisha utu wako mzima na kuwasha moto katika mawazo, fikra na hisia zako zote, kiasi cha kuhisi unampapasa na kumwona Mungu katika Roho na kuwa halisi.

*1Yoh1.1-2, Lile lililokuako tangu mwanzo tulilolisikia, tulililoliona na macho yetu tulilolitazama, na mikono yetu ikalipapasa kwa habari ya neno la uzima na uzima huo ulidhihirika nasi tumeona tena twashuhudia huo uzima.Uhalisi huu unampeleka mtu kumwabudu MUNGU.*

**Angalizo:-**
– Ibada lazima ifanywe katika roho. Hamasiko liwe la Roho Mtakatifu na siyo misisimko ya mwili na akili tu.
– Ibada ifanyike katika moyo wa dhati na wa kweli iliyofunuliwa na Yesu yaani sawasawa na NENO lake.

Wakati wa kuabudu ni wakati muhimu mno, ni wakati wa shughuli ya utukufu kupita zote ambazo mwanadamu anafanya katika maisha yake, wakati wa kuabudu unazidi nyakati zote anazoweza kuzifurahia, tena kuabudu huacha kumbukumbu ndani yake, kumbukumbu ya kuabudu inapita vilele vyote vya furaha hizo maana ni wakati wa kukutana na Mungu. Je mwanadamu ninani hata akapewa nafasi tukufu kama hiyo? Kwakuwa, kuabudu ni sehemu ya maisha na ushirika na Mungu na ni jambo la rohoni, basi, kuabudu kunakuwa sehemu ya kila jambo analofanya, na ni ufunguo wa maisha yenye mafanikio na mwelekeo wa fikra na mawazo ya moyo, na kuwa mtindo wa maisha

**2.5 KUABUDU NA MAOMBI**

Maombi ni njia kuu na bora zaidi ya kumsifu na kumwabudu Mungu. Maombi ni wakati ambao mtu anazungumza na Mungu mambo yake na kujimimina moyo wake mbele za Mungu. Katika maombi ya dhati na ya kweli, mtu hujiachia akawa wazi kujieleza na kutoa siri za moyo wake akijua Mungu ndiye msaada wake na kimbillio lake. Zab. 46:1-3 Kwa kutambua ukuu wa Mungu na uwezo wake ndipo ibada ya kweli toka vilindi vya moyo huanza, na mtu hushuka chini sana katika ufahamu wake kumtambua Mungu ni nani na kumwabudu na kumpa sifa katika maombi. Katika hali hiyo ya maombi humfanya mtu ajione si kitu bali astahiliye ni Mungu, ndipo wengine huanguka chini na kugaragara kuonyesha upendo mbele za Mungu. Math 26: 39 Luka 22: 44, Ay 19: 25 -27 Hata malaika wanaabudu na kuanguka mbele za Mungu. Yesu naye aliabudu hata akalia na kutoa machozi ya damu akiomba. Ayubu aliomba na kujiachia mikononi mwa Mungu akisema, najua mtetezi wangu yu hai na pasipo mwili huu nitamwona Mungu. Maombi huvuka mipaka ya mazingira ya mwili wa nyama na kumleta mtu mahali alipo Mungu katika Roho kiasi kwamba muombaji anakuwa na mazungumuzo na Mungu ana kwa ana kama Paulo asemavyo ABA yaani Baba aliye karibu naye kama mwana.

## 3. BWC KAMA KITUO [KANISA]

**KANISA**

### 3.1 Chimbuko la Kanisa

Biblia hulionyesha kanisa kuwa ni taasisi ya kimbingu, ikiliita Kanisa la Mungu (Mdo.20:28), 1Kor.1:2), Yesu aliwekeza mamlaka yake ndani ya Kanisa (Mt. 18:1, 18). Twaweza kutambua mizizi ya Kanisa katika Agano la Kale na vielelezo vya Agano Jipya.

### 3.2 Maana ya Kanisa Kibiblia

Kwenye Biblia, neno la Kigiriki lililotafsiriwa kanisa ni *ekklesia*, likimaanisha kuitwa ili kuondoka/kutoka. Kitabu kiitwacho Septuagint yaani tafsiri ya Kigiriki ya Agano la Kale iliyotumiwa

nyakati za Yesu, hutafsiri neno la kiebrania *qahal* iliyomaanisha mkutano, kusanyiko, jamii. (Kumb 9:10, 18:16; 1Sam 17:47, 1Waf 8:14, 1Nya 13:2).

**AGANO JIPYA AMBAKO MAANA ZIFUATAZO ZA KANISA ZINAIBULIWA KAMA IFUATAVYO:-**

**(1)** Waumini wanaokutana kuabudu katika mahali Fulani maalum (1Kor. 11:18; 14:19, 28)
**(2)** Waumini wanaoishi katika eneo mojawapo kijiografia (1Kor.16:1, Gal.1:2 1Thes.2:14)
**(3)** Kundi la waumini katika nyumba ya mtu (1Kor.16:19, Kol. 4:15, Filem. 2)
**(4)** Makundi ya Makusanyiko ya waumini kwenye eneo mojawapo kijiografia (Mdo. 9:31)
**(5)** Kundi linalojumuisha waumini wote ulimwenguni (Mt. 16:18; 1Kor.10:32; 12:28; cf. Efe. 4:11-16)
**(6)** Jamii ya waumini waaminifu wote ulimwenguni duniani na mbinguni (Efe. 1:20-22; Filip. 2:9-11)

**3.3 Mizizi ya Kanisa**

Agano la Kale linadhihirisha kwamba kanisa ni kundi lenye mpangilio la watu wa Mungu. Tangu awali familia zenye kumcha Mungu tangu Adamu, Seti, Nuhu, Shemu na Ibrahimu ziliutunza ukweli. Mungu alitoa ahadi nzito na hatimaye hii nyumba ya Mungu ilikuwa taifa: na jamaa zote zote za dunia watabarikiwa (Mwa. 12:1-3) Taifa alilolitoa Misri liliitwa Kanisa llililokuwa Jangwani (Mdo. 7:38). Washiriki wake wa Kanisa walitambulika 'ufalme wa makuhani na taifa takatifu (Kut.19:6), Watakatifu wa Mungu (Kumb.28:9 c/f Law.26:12), Kanisa lake. Aliwaweka Palestina, mahali ambako mabara matatu ya Afrika, Ulaya na Asia hukutana lengo likiwa kuwaita wote waingie (Isa.56:7). Pamoja na uangalizi wa Mungu, Israeli waliendelea kuabudu miungu mingine, kujitenga kiubaguzi, utaifa, kiburi na kujiangalia wenyewe, wakashindwa kutimiza makusudi ya Mungu.

Katika siku za Yesu, Israeli walipata upendeleo wa kufikiwa na Masihi aliyetarajiwa kuwafungua kwenye utumwa wa kujitumainia nafsi. Kwa kumsulibisha Yesu, ilidhihirika jinsi Israeli walivyooza ndani yao. Walipopaza sauti hatuna mfalme ila Kaisari (Yoh. 19:15), walikataa Mungu asitawale juu yao. Kwa kushindwa Israeli, Mungu alianzisha taifa jingine, kanisa jingine, ambalo lingetimiza makusudi yake. (Mt. 21:41,43).

Kanisa katika Agano jipya linaundwa na Wayahudi waumini na watu wa Mataifa mengine (Gal.3:26-29). Wayahudi wasiomwamini Yesu siyo watoto wa Mungu tena (Rum.9:6-8). Mataifa wanaomkubali Mungu wanafananishwa na mzabibu mwitu ulipandikizwa kwenye mzabibu mwema (Rum.11:17-25). Matawi yanaonywa kushikamana na Mungu wasije wakakatiliwa mbali (Rum.11:16-18). Tofauti na Kanisa kwenye Agano la Kale, Kanisa la Agano Jipya halijifungamanishwi na taifa moja, bali limepangiliwa kuwa la Ulimwengu mzima (Mt.28:19)

**3.4 Vielelezo vya Agano Jipya Kuhusu Kanisa**

***3.4.1 Kanisa kama Mwili:*** *Kanisa kama mwili ni kielelezo kinachosisitiza umoja wa Kanisa na* mahusiano baina ya washiriki. Msalaba huwapatanisha waumini katika mwili moja (Efe.2:16). Kwa njia ya Roho Mtakatifu hubatizwa katika mwili moja (1Kor.12:13). Mwili unaosemwa hapa ni wa Yesu

Kristo (Efe.1:22, 23). Washiriki ni viungo kwenye mwili wa Kristo (Efe.5:30). Kristo ndiye huhuisha mwili wake. Yeye ndiye kichwa (Kol.1:18) kiongozi wa Kanisa (Efe.5:23).

***3.4.2 Kanisa kama Hekalu:*** Kanisa ni hekalu, maskani ambako Roho Mtakatifu hukaa. (1Kor. 3:9-16, Efe.2:20). Hekalu hili liko hai, kwa kuwa Kristo ni jiwe lililo hai na washiriki mawe yaliyo hai ambayo hufanya nyumba hai. (1Pet. 2:4-6). Hekalu halijakamilika, linaendelea kujengwa (Efe.2:22) na zana bora zatakiwa kulijenga ili listahimili majaribu hata hukumu (1Kor.3:12-15). Kielelezo cha hekalu husisitiza utakatifu kwa kuwa atayeliharibu ataharibiwa (1Kor.3:17). Hakuna ushirika baina ya Kristo na Beliari (2Kor. 6:14, 16).

***3.4.3 Kanisa kama Bibi Arusi***: Kanisa husemwa kuwa Bibi Arusi wa Bwana Harusi Yesu Kristo. Bwana asema nitakuposa uwe wangu milele (Hosea 2:19), Mimi ni mume wenu (Yer.3:14). Paulo anarudia kielelezo hiki kwa kusema nalimposea Kristo bikira safi (Kol.11:2). Upendo wa Kristo kwa kanisa ni mkubwa kwani alilazimika kufa kwa ajili yake(Efe.5:25) na kwa kafara yake kulisafisha (Efe.5:26) ni sala yake litakaswe kwa neno (Yoh.17:17) ili hatimaye liwe safi na lisilo na mawaa (Efe.5:27).

***3.4.4 Kanisa kama Yerusalemu iliyo juu****:* Biblia huita jiji la Yerusalemu Sayuni. Humo, Bwana anakaa na watu wake (Zab.11:9), na wokovu hutokea (Zab.14:7, 53:6). Ni furaha ya dunia yote (Zab.48:2). Agano jipya hutambua jiji la Yerusalemu la juu mbinguni (Gal.4:26) na wakazi wa Yerusalemu hiyo wana makazi na uraia wa mbinguni (Wafil.3:20). Wakazi ni wana wa ahadi, waliozaliwa kwa roho (Gal. 4:28, 29; 5:1), hawajitahidi kuhesabiwa haki kwa matendo ya sharia (Gal.4:22, 26, 31; 5:4) bali kwa imani. Wanatambua kwamba imani itendayo kwa upendo ndiyo huwapa uraia (Gal. 5:5, 6). Waliofika hapo, wako kwenye maskani ya Mungu yenye malaika maelfu na majina yao yameandikwa kuwa ni wenyeji (Ebr.12:22, 23).

## 4. ADUI WA MKRISTO KATIKA KUMWABUDU MUNGU

1. **Shetani:** ni adui yetu mkubwa na hupenda kuona watu wa dunia hii wakimtukuza yeye kwa kuwajaribu na fahari za dunia hii na kukamata muda wao ili waone mahitaji ya mwili ni muhimu sana kuliko kumtumikia Mungu wa kweli.Tunaona namna shetani alipomjaribu Yesu kwa kumpandisha juu na kumwonyesha miliki zote za dunia na atampa zote ikiwa atamsujudia *(Luka4:6-7- Ibilisi akamwambia Nitakupa wewe Enzi hii yote na fahari yake kwa kuwa imo mikonani mwangu nami humpa ye yote kama nipendavyo.Basi wewe ukisujudu mbele yangu yote yatakuwa yako).*
2. **Mwili:** Mara nyingi mwili hupingana na roho kwa kuleta vishawishi vya kufanya lile ambalo hupendi kulitenda.Ndiyo maana utakuta wakristo wengi siyo watendaji wa Neno.Mtume Paulo alilia kwa sababu ya mwili wa mauti *(Roma7:18 Kwa maana najua ya kuwa ndani yangu, yaani ndani ya mwili wangu, halikai neno jema, kwa kuwa kutaka nataka bali kutenda lililo jema sipati)*

3. **Kujivuna:** Watu wengi wamejaa majivuno,viburi na njia mbovu kiasi kwamba hawana muda na hawezi kuona thamani ya kujitoa kwa Mungu aliyewaumba katika kumwabudu kwa

unyenyekevu.Mungu anachukia kiburi,majivuno,uovu,kinywa cha ukaidi pia anakichukia *(Mithali 8:13 Kumcha Bwana ni kuchukia uovu; Kiburi na majivuno, na njia mbovu, Na kinywa cha ukaidi pia nakichukia).*

4. **Mapokeo:** Kuna wakristo wengi wanendelea kuabudu mapokeo ya dini na wanashindwa kuabudu Mungu katika njia ya kweli kwa sababu ya upofu wao katika kuijua Habari Njema (*1Korintho2:14 Ila Mungu ashukuriwe, anayetushangiliza daima katika Kristo, na kuidhihirisha harufu ya kumjua yeye kila mahali kwa kazi yetu).*

   Mungu anapenda tumwabudu katika roho na kweli namna ambayo yamfaa Mungu.Maisha yetu yaonyeshe kwa mataifa kuwa tunamtegemea Mungu na kuweka imani ndani yake-kwamba yeye amefanya kila lililopendeza duniani na mbinguni, na yeye ndiye anayestahili kuheshimiwa. Yeye ndiye nguvu yetu na msaada wetu katika maisha yetu. Tusiabudu watu, kazi, mali, dhehebu, siku, sikukuu, sanamu au chochote kile bali tumwabudu Mungu katika roho na kweli ambayo ni njia pekee tunayoweza kumpendeza Mungu wetu katika maisha yetu ya sasa na mwisho wake tupate uzima wa milele.

5. **BWC Tunaamini**

